

Kuza biashara yako kupitia huduma ya “Mkopo Kocha” inayotolewa na Programu ya ENGINE

Huduma ya “Mkopo Kocha” kupitia programu ya ENGINE inawaongezea wamiliki wa biashara nafasi ya kufanikiwa kupata mikopo

ENGINE (Programu ya kuwezesha ukuaji kupitia uwekezaji na biashara), inasaidia wamiliki wa biashara waliopo Zanzibar na mikoa ya Mbeya, Morogoro na Iringa kwa kuwaunganisha na washauri wa biashara waliopewa mafunzo maalum ya “Mkopo Kocha” ili kuwaongezea nafasi ya kufanikiwa kupata mikopo.

PATA PUNGUZO

Uliza mshauri wa “Mkopo Kocha” kama unasifa ya kupata eCoupon kupitia programu ya ENGINE, ili kupunguza gharama ya huduma hii

Inavyofanya Kazi



HATUA YA 1: TAFUTA MSHAURI WA “MKOPO KOCHA”

Tembelea tovuti ya Bizfundi www.bizfundi.or.tz na usajiri biashara yako, kisha tafuta washauri wa “Mkopo Kocha” walioteuliwa maalum kwa shughuli hiyo.



HATUA YA 2: TATHMINI

Mshauri atatathmini biashara yako na kisha kukueleza gharama za huduma.



HATUA YA 3: TEKELEZA MPANGO WAKO

Kwa pamoja wewe na mshauri wako mtatengeneza na kuandaa matarajio ya mapato halisi, taarifa za fedha na nyaraka zinazohitajika.



HATUA YA 4: JIUNGE NA TAASISI YA FEDHA

Ukishakamilisha, maelezo yako ya biashara yatawekwa kwenye mtandao wa taasisi za kifedha zitakazotathmini na kuonesha kama watapenda kufanya kazi na wewe.



HATUA YA 5: OMBA MKOPO

Jiunge Leo

ENGINE iko tayari kukuwezesha kukuza biashara yako. Wasilisha ombi lako kwa Mshauri wa Biashara LEO!

KUJIUNGA, TEMBELEA WWW.BIZFUNDI.OR.TZ AU TAFUTA “BIZFUNDI” KWENYE GOOGLE PLAY STORE

TEMBELEA WWW.BIZFUNDI.OR.TZ BARUA PEPE BIZSUPPORT@IESC.ORG PIGA SIMU +255-752-180-961

ENGINE ni programu ya miaka minne inayofadhiliwa kupitia “Feed the Future” na USAID. Inatekelezwa na IESC kupitia “Volunteers for Economic Growth Alliance”. “Feed the Future” ni mpango toka serikali ya Marekani kuthibiti njaa duniani. Ikiwalenga wakulima wadogo wadogo, hasa wanawake, “Feed the Future” inasaidia nchi washirika kuendeleza sekta za kilimo ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi na biashara kuongeza kipato na kupunguza njaa, umaskini na utapiamlo. USAID ni wakala wa serikali ya Marekani anayeongoza kufanya kazi ya kukomesha umaskini uliokithiri duniani na kuwezesha ustahimilivu katika jamii ili zitambue uwezo wao.